




Kuangalia Kupatwa kwa Jua nchini Tanzania
On Observing the Solar Eclipse in Tanzania

Alfajiri ya 21 Juni, 2020

Dawn of June 21, 2020

by Eliatosha Maleko
edited by Mponda Malozo



Source: [Cmglee](#) courtesy of [Wikipedia](#)

Local Type: Partial Solar Eclipse, in Arusha

Begins: Sun, Jun 21, 2020 at 6:46 am

Maximum: Sun, Jun 21, 2020 at 7:46 am 0.62 Magnitude

Ends: Sun, Jun 21, 2020 at 8:55 am

Duration: 2 hours, 9 minutes



Kuangalia Kupatwa kwa Jua nchini Tanzania

Kwa kawaida, Jua hupatwa mara mbili hivi kila mwaka, na hilo hutokea wakati ambapo Mwezi, Jua na Dunia vinakuwa katika mstari ulionyooka. Wakati wa kupatwa Mwezi hukatiza kati kati ya Dunia na Jua na hivyo kuzuia mwanga wa Jua kufika Duniani kwa kutengeneza kivuli katika sehemu ya uso wa Dunia.

Unaweza kutengeneza jaribio lako nyumbani kwa kuwa na chanzo cha mwanga kama tochi na kitu cha duara mfano chungwa na kuona jinsi chungwa linavyoweza kuzuia mwanga na kutengeneza kivuli mbele ya chanzo cha mwanga, hata likiwa mbali. Ukiweza kufanya jaribio hili unaweza kututumia picha nasi tutaichapisha kwenye tovuti yetu.

Kupatwa kwa jua inatarajiwa mwanzoni mwa Juni 21, 2020, katika nchi nyingi ikijumuisha Tanzania. Hafla hii ya kupatwa kwa jua itakuwa ya sehemu kwa watazamaji kutoka Tanzania na nchi kadhaa barani Afrika na Asia.

Kuna aina mbali mbali za kupatwa kwa Jua kutokana na umbali uliopo Mwezi kutoka Duniani. Kupatwa kwa wakati huu hapatakuwa kamilifu kwa kutakuwa na sehemu ndogo ya Jua ambayo haitazibwa kabisa na Mwezi hata kwa watu wakaoshuhudia kupata kikamilifu.

Nchini Tanzania hatutaona kupatwa kikamilifu hata wakati wa kilele ila tutaweza kuona sehemu ya Jua inavyopatwa na jinsi Mwezi utakavyokuwa unakatisha katika uso wa Jua.

Kamwe usiangalie kupatwa kwa Jua kwa macho yako au darubini bila miwani maalum au kizuizi cha kuchuja mwanga wa Jua na miale ya Infrared na Ultra violet kutoka kwenye Jua. Utaharibu macho yako.

Jumuiya ya Astronomia Afrika imeandaa kitabu maalumu chenye taarifa muhimu kuhusu kupatwa kwa Jua na njia za salama za kushuhudia tukio la kupata kwa Jua kwa njia salama ukiwa nyumbani. Pakua kitabu hiko kwa kubonyeza [hapa](#).

The Mt. Meru Astronomical Observatory kinashirikiana na jumuiya ya Astronomi Afrika kutafsiri kitabu hiko pamoja na program maalumu ya simu za Android App kwa Kiswahili.

Endelea kufuatilia [ukurasa wetu wa Facebook](#) na [kutembelea tovuti yetu](#) ili kufahamu upatikanaji wa tafsiri hizo mara baada ya kukamilika na pia taarifa mbali mbali kuhusu elimu ya astronomia na matukio ya kuangalia anga na elimu katika kituo chetu.

By Eliatosha Maleko





Solar Eclipse on the Dawn of 21st June In Tanzania

Normally, solar eclipse event occurs about two times in a year, when the Moon, the Sun and the Earth are in a straight line. During the eclipse the Moon moves between the Earth and the Sun, casting a shadow across a portion of the surface of the Earth.

You can design an experiment at home using a source of light source such as a flashlight and a circular object such as an orange, to see how an orange can block the light from its source, even if at a distance. If you try this, you can share with us a picture and we will post it on our website.

The eclipse is expected in the dawn of June 21, 2020, visible in many countries including Tanzania. This eclipse event will be partial for viewers from Tanzania and some countries in Africa and Asia.

There are different types of solar eclipses, determined by the distance of the Moon from the Earth. The eclipse at this time will not be a total eclipse, but annular eclipse, where small part of the Sun will not be obscured by the Moon even for people who will be at the center of the eclipse path.

In Tanzania we will not see total eclipse even at climax, but we will see part of the Sun covered by the Moon as it passes in front of the Sun.

Never look at the eclipse with your naked eye or through the telescope or lens without special special filters of glasses to filter the visible, Infrared and Ultraviolet lights from the Sun. You will damage your eyes.

The African Astronomical Society has prepared a special book containing important information about the eclipse and the safest ways to observe the event at home.

Download the book here:

drive.google.com/file/d/1OtdbVEgyXaJah_Tveg8VF7PGwUoJRG-S/view

The Mount Meru Astronomical Observatory, in collaboration with the African Astronomical Society are translating the book and an Android App in Kiswahili for viewers in Tanzania and Swahili speakers.

Follow us on our [Facebook page](#) and [visit our website](#) to get the translated version finalized and to be updated on important astronomical updates, astro-education activities going on at our observatory.

Translated by Mponda Malozo

More information, charts, diagrams, and animations, available at:

<https://www.timeanddate.com/eclipse/solar/2020-june-21>

For information specific to the Arusha location:

<https://www.timeanddate.com/eclipse/in/tanzania/arusha>

For further information, diagrams, and explanations visit the African Astronomical Society's on-line resources for the [June 21, 2020 Annular Solar Eclipse](#).